

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِينَ مَأْتُوا مِنْكُمْ وَعَجِلُوا الصَّدَقَاتِ لِيَسْتَخْفَفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيَسْكُنَنَّ لَهُمْ دِيْنُهُمُ الَّذِي أَرْتَهُمْ لَهُمْ وَلَيَسْبِئَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَرْقِهِمْ أَنَّا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ فِي شَيْءٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّاهِرُونَ



Jumatatu, 9 Safar 1444 H

05/09/2022 M

Na: 1444 / 04

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

(مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رَجُلٌ صَدَقَوَا مَا عَاهَدُوا اللّٰهُ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَنْ قَضَى نَحْبَةً
وَمِنْهُمْ مَنْ يُنْتَظَرُ وَمَا بَلَّوْا تَبَدِيلًا)

“Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.” [Al-Ahzab: 23]

Kwa imani na kujisalimisha kwa qadhaa ya Mwenyezi Mungu (swt), Hizb ut Tahrir/Wilaya ya Jordan inaomboleza kwa Waislamu kwa jumla, na watu wa Jordan haswa, na kwa Amir wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata bin Khalil Abu Al-Rashtah, mmoja wa mashababu wake wanyofu, wavumilivu, na mashuhuri, na mwenye misimamo thabiti inayomridhisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake (saw), na wala hatumtakasi yejote mbele ya Mwenyezi Mungu:

Mwanachuoni wa fiqhi na mwanafikra wa kisiasa kutoka kizazi cha kwanza cha mashababu wa Hizb ut Tahrir

Muhammad Hussein Abdulla (Abu Sufyan)

Ambaye amekwenda kwa rafiki yake aliyeko juu (swt), leo Jumatatu, tarehe 5/9/2022 M, baada ya maisha alioishi katika utiifu kwa Mwenyezi Mungu (swt), akibeba ulinganizi wa haki na kheri pamoja na Hizb ut Tahrir tangu kuasisiwa kwake, akifanya kazi ya kuregesha maisha kamili ya Kiislamu kuitia kusimamisha Dola ya Khilafah kwa njia ya Utume, akiwa mvumilivu kwa aliyokutana nayo kwa ajili ya hili, ikiwemo kuteswa, kukamatwa na kufungwa gerezani, kwa hayo akitarajia mema kwa Mwenyezi Mungu, akiwa na thiqa na nusra yake (swt), na yeye Mwenyezi Mungu amrehemu akabakia thabiti juu ya haki ambayo alibeba, akisafiri kwa ukakamavu, asiyeyumba na asiyeteteleka katika azimio lake, aliyejaa imani kwa ahadi yake (swt) kwa Umma wa Kiislamu kwa nusra na tamkini.

Twamuomba Mwenyezi Mungu amfinike marehemu wetu, marehemu wa umma, kwa rehema zake, na amjaaliye kwa mapokezi mema, na amjaalie makaazi yake katika Pepo ya juu kabisa ya Firdaus pamoja na mitume, wakweli, mashahidi, na wema na hao ndio marafiki wema, na kumlipa kwa niaba yetu na kwa niaba ya Uislamu na Waislamu malipo bora zaidi, kama ambavyo twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwa ajili yetu na familia yake subira na faraja njema.

(إِنَّا لِلّٰهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ)

“Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqara: 156]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Jordan**